JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

BODI YA USAJILI WA WATAALAM WA MIPANGOMIJI

SIFA NA MAHITAJI WAKATI WA KUOMBA USAJILI

Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, ni Taasisi ya Serikali iliyoundwa chini ya Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji Sura ya 426 RE. 2023. Mojawapo ya jukumu la Bodi ni kusajili Wataalamu wa Mipangomiji pamoja na Kampuni zinazofanya kazi za Mipangomiji.

Bodi inapenda kuwatangazia Wataalamu wa Mipangomiji waliohitimu Taaluma ya Mipangomiji kujisajili ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, taratibu na Kanuni. Sifa za kuomba usajili kwa kila kundi la usajili zimeainishwa hapa chini.

A. USAJILI WA AFISA MIPANGOMIJI MSHAURI (CONSULTING TOWN PLANNER)

1. Barua ya maombi ya usajili
2. Kitambulisho cha uraia (NIDA)
3. Mwombaji awe na uzoefu kama Afisa Mipangomiji kamili (fully registered town planner) usiopungua miaka 10.
4. Awe ameonesha uadilifu na weledi katika kutekeleza kazi za Mipangomiji.
5. Awe hajawahi kukutwa na hatia ya udanganyifu, kukwepa kodi na makosa mengine ya kukiuka maadili ya taaluma ya Mipangomiji.
6. Risiti ya ada ya maombi ya usajili:
    a) Sh. 300,000 kwa raia wa Tanzania.
    b) Shilingi za kitanzania zenye thamani sawa na USD 2,500 kwa wasio raia.
7. Fomu ya Maombi ya Usajili (nakala mbili) – inapatikana katika tovuti ya TPRB: http://www.tprb.go.tz
8. Maombi ya usajili ya kundi hili yatumwe kwa Barua pepe ya Msajili: registrar@tprb.go.tz

B. USAJILI KAMILI (FULLY REGISTERED TOWN PLANNER)

1. Barua ya maombi ya usajili
2. Kitambulisho cha uraia (NIDA)
3. Mwombaji awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu (3) wa vitendo kama Mtaalamu wa Mipangomiji.
4. Kazi tatu (3) za Mipangomiji zilizoidhinishwa pamoja na taarifa zake za kitaalamu (*planning briefs)*.
5. Fomu ya Maombi ya Usajili (nakala mbili) – inapatikana katika tovuti ya TPRB: http://www.tprb.go.tz.
6. Vyeti vya taaluma (Chuo Kikuu, Kidato cha 6 na Kidato cha 4) pamoja na cheti cha matokeo (*transcript)* ya Chuo Kikuu.
7. Wasifu wa sasa wa mtaalam (*CV*).
8. Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN).
9. Picha mbili (2) za rangi (pasipoti)
10. Risiti ya ada ya maombi ya usajili:
    a) Sh. 100,000 kwa raia wa Tanzania.
    b) Shilingi za kitanzania zenye thamanisawa na USD 1,500 kwa wasio raia.
11. Maombi ya usajili ya kundi hili yawasilishwe, katika nakala ngumu (hard copy); kwa Msajili, Bodi ya Usajiliw a Wataalamu wa Mipangomiji, S. L. P 1150, Dodoma.

C. Afisa Mipangomiji Mhitimu (Graduate Town Planner)

1. Barua ya maombi ya usajili
2. Awe Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Kitambulisho cha Uraia-NIDA)
3. Awe amehitimu shahada ya kwanza ya Mipangomiji katika chuo kinachotambuliwa na Serikali
4. Ajaze fomu nakala 2 za maombi ya usajili
5. Uthibitisho wa malipo ya Ada ya maombi ya Usajili (Tanzania shilingi) 75,000/=
6. Wasifu (Curriculum Vitae)
7. Aambatanishe picha 2 za rangi (Current colored passport size)

8. Aambatanishe vyeti vya taaluma na matokeo (Academic certificate and Transcript)
9. Maombi ya usajili ya kundi hili yatumwe kwa Barua pepe ya Msajili: registrar@tprb.go.tz

D. AFISA MIPANGOMIJI MSAIDIZI (Technician Town Planner)

1. Barua ya maombi ya usajili
2. Awe Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Kitambulisho cha Uraia-NIDA)
3. Awe amehitimu Astashahada ya Mipangomiji katika chuo kinachotambuliwa na Serikali
1. Ajaze fomu nakala 2 za Maombi ya Usajili
2. Uthibitisho wa malipo ya Ada ya Maombi ya Usajili Shilingi 50,000/=
3. Wasifu (Curriculum Vitae)
4. Aambatanishe picha za rangi 2 (current colored passport size)
5. Aambatanishe vyeti vya taaluma na matokeo (Academic certificate and Transcript)
6. Awe amefaulu Mtihani uliotolewa na Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipangomiji
7. Maombi ya usajili ya kundi hili yatumwe kwa Barua pepe ya Msajili: registrar@tprb.go.tz

---

E. USAJILI WA KAMPUNI

1. Barua ya maombi ya usajili
2. Maafisa Mipangomiji wawili (2) wenye usajili kamili, ambapo mmoja wao ni Mkurugenzi na mmiliki mwenye hisa nyingi, au Maafisa Mipangomiji wawili wenye usajili kamili Pamoja na kumiliki hisa zaidi ya asilimia 50.
3. Nakala ya vyeti vya usajili kwa Maafisa mipangomiji ambao ni Wakurugenzi.
4. Picha mbili (2) za rangi za wakurugenzi (pasipoti) za hivi karibuni.
5. Wasifu wa sasa wa wakurugenzi (CV).
6. Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN).
7. Leseni ya biashara iliyotolewa na mamlaka husika.
8. Cheti cha usajili wa kampuni kutoka mamlaka husika
9. Fomu ya Maombi ya Usajili (nakala mbili) – inapatikana katika tovuti ya

TPRB: http://www.tprb.go.tz

10. Wasifu wa sasa wa kampuni (*Company Profile*).
11. Katiba na Kanuni za Kampuni (*Memorandum & Articles of Association*) - zioneshe kuwa kazi kuu ya kampuni ni kazi za upangaji miji.
12. Uthibitisho wa kuwa na ofisi ya kazi za mipangomiji.
13. Risiti ya ada ya usajili:

a) Sh. 350,000 kwa kampuni za ndani.

b) **Dola 2,200** kwa kampuni za kigeni.

14. Masharti ya ziada kwa kampuni za kigeni:

a) Uthibitisho wa usajili katika nchi ya asili kabla ya kuja Tanzania.

b) Uthibitisho wa kuteuliwa kufanya kazi ya Mipango miji nchini Tanzania.

c) Kibali cha kazi nchini kutoka mamlaka husika.

d) Uthibitisho wa kushirikiana na kampuni ya ndani ya Mipango miji iliyosajiliwa.

e) Katiba ya kampuni ioneshe kuwa kazi kuu ni Mipango miji.

f) Kiapo kinachoonesha kuwa usajili utasitishwa mara baada ya kazi ya mipangomiji aliyoteuliwa kufanya kukamilika.

TANBIHI

- Malipo yote yafanywe kupitia Namba ya Malipo ya Serikali (Control Number) inayopatikana katika mfumo wa Ankara wa bodi: https://billing.tprb.go.tz.
- Kwa mawasiliano zaidi:

Simu: +255 (026) 232 3833 | +255 739 504 222

Baruapepe: registrar@tprb.go.tz

Tovuti: www.tprb.go.tz

- Maombi ya usajili wa kampuni ya mipangomiji yaliyofanywa na mtaalamu mwenye usajili kamili lakini ana deni la ada ya mwaka hayatashughulikiwa hadi atakapolipa deni hilo.